



TAARIFA ZA RAMANI YA ENEO TAMBARARE LA MAFURIKO YA KAUNTI YA HENRICO MASWALI YANAYOULIZWA SANA

Kaunti ya Henrico ilishiriki katika mchakato wa miaka mingi na Shirika la Udhibiti wa Dharura la Nchi (Federal Emergency Management Agency, FEMA) ili kuunda ramani ya maeneo yake ya sasa yanayoweza kuathiriwa na mafuriko. Ramani hizo, zinazojulikana kama Ramani za Kiwango cha Bima ya Mafuriko (Flood Insurance Rate Maps, FIRMs), zitaanza kutumika tarehe 25 Aprili 2024.

Hati hii ya maelezo imetayarishwa ili kusaidia kujibu maswali ya wakazi na wamiliki wa biashara kuhusu mchakato, ratiba, athari na chaguo zinazohusiana na ramani mpya za hatari ya mafuriko za FEMA, ikiwa ni pamoja na mahali pa kwenda ili kupata habari zaidi.

1. Ramani za hatari ya mafuriko ni nini?

Ramani za hatari ya mafuriko, zinazoitwa pia Ramani za Kiwango cha Bima ya Mafuriko (Flood Insurance Rate Maps, FIRMs), zinaonyesha viwango vya hatari ya mafuriko na ni zana muhimu katika juhudi za kulinda maisha na mali katika Kaunti ya Henrico. Zikiwa zimeundwa na FEMA kwa ajili ya udhibiti wa mafuriko na mipango ya jamii, ramani hizi zinaonyesha maeneo ya mafuriko ya jamii, Mwinuko wa Mafuriko ya Msingi (Base Flood Elevations, BFEs), na mipaka ya eneo tambarare la mafuriko.

2. Kwa nini Kaunti ya Henrico inapata ramani mpya za hatari ya mafuriko?

Ramani za sasa za mafuriko za Kaunti ya Henrico zimepitwa na wakati, kwa kuwa zinategemea data na mbinu za kuanzia mwaka wa 2007 na miaka ya nyuma. Baada ya muda, mtiririko wa maji na mifumo ya mifereji ya maji inaweza kubadilika sana kutokana na mmomonyoko wa ardhi, maendeleo na sababu za asili. Uwezekano wa kutokea kwa mafuriko katika maeneo fulani umebadilika pamoja na sababu hizi.

Ramani mpya za mafuriko zinajumuisha data mpya na teknolojia mbinu mpya kabisa ili kutoa picha iliyosasisiwa ya hatari ya mafuriko ya Kaunti ya Henrico. Matokeo yake - taswira bora ya maeneo ambayo yanaweza zaidi kuathiriwa na mafuriko na msingi bora wa kufanya maamuzi muhimu.

3. Ni nani anayefaidika na ramani mpya za hatari ya mafuriko?

Kuwa na ramani za sasa na sahihi zaidi kutanufaisha vikundi vingi kwa njia tofauti:

Unapaswa Kujua

Zaidi ya utathmini wa hatari ya mafuriko na ramani iliyotayarishwa na FEMA, Kaunti ya Henrico ina maeneo ya ziada yanayoweza kuathiriwa na mafuriko ambayo yamewekwa kwenye ramani na yanajulikana kama Maeneo Maalum ya Hatari ya Mafuriko ya Jamii (Community Special Flood Hazard Areas, SFHAs). Maeneo haya hayasasisiwi kama sehemu ya sasisho hili la ramani ya eneo la FEMA, lakini yanasasisiwa na yanatarajiwa kukamilika mwaka wa 2025. Pata maelezo zaidi katika henrico.gov/works/design/floodplain/map-updates. Angalia pia swali la 8 ili upate maelezo zaidi kuhusu Maeneo Maalum ya Hatari ya Mafuriko Yaliyotambuliwa na Kaunti (County-identified Special Flood Hazard Areas) na msharti maalum kuhuyahusu.

- Wakazi na wamiliki wa biashara watakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi bora kuhusu kupunguza hatari yao na kulinda mali zao kwa bima kutokana na athari za kifedha za mafuriko.
- Wapangaji wa jamii na maafisa wa eneo wataelewa zaidi hatari za mafuriko na hatari zinazoathiri Kaunti ya Henrico, ili waweze kuboresha shughuli za mpango wa eneo.
- Wajenzi na watengenezaji watapata habari zaidi za kina za kufanya maamuzi kuhusu mahali pa kujenga na jinsi ujenzi unaweza kuathiri maeneo ya eneo yanayoweza kuathiriwa na hatari ya mafuriko.
- Watoa huduma za bima, mali isiyohamishika na ukopeshaji wataweza kufikia taarifa kwa urahisi mtandaoni na mabadiliko yajayo ili kuwahudumia wateja wao na jamii kwa ufanisi zaidi.

4. Ni nini maana ya eneo lenye hatari kubwa, na ninawezaje kutambua ikiwa mali yangu iko katika eneo hili?

Katika Kaunti ya Henrico, maeneo yenye hatari kubwa ya mafuriko yanatambuliwa kama SFHA, ambayo yanajumuisha maeneo ya SFHA ya FEMA na maeneo ya SFHA ya Jamii. Maeneo haya mara nyingi yanajulikana kama maeneo tambarare ya mafuriko au maeneo yaliyo katika "eneo la mafuriko la miaka 100." Neno "mafuriko ya miaka 100" linaweza kupotosha. Inaelezewa kwa usahihi zaidi kuwa mwinuko wa eneo la mafuriko ambao una uwezekano wa asilimia 1 wa kufikiwa au kufunikwa na mafuriko kila mwaka. Si mafuriko ambayo yatatokea mara moja kila baada ya miaka 100. Hakuna njia ya kutabiri wakati ambapo mafuriko yajayo yatatokea—au yatakayotokea baada ya hayo.

Tembelea henrico.gov/works/design/floodplain/map-updates ili upate maelezo zaidi na uone ramani za sasa na mpya. Tovuti pia ina maelezo kuhusu ya matukio yajayo na nyenzo nyingine muhimu zinazohusiana na mafuriko.

VIFUPISHO

BFE (Base Flood Elevation) – Mwinuko wa Mafuriko ya Msingi

FEMA (Federal Emergency Management Agency) – Shirika la Udhibiti wa Dharura la Nchi

FIRM (Flood Insurance Rate Map) – Ramani ya Kiwango cha Bima ya Mafuriko

LOMA (Letter of Map Amendment) – Barua ya Marekebisha ya Ramani

LOMC (Letter of Map Change) – Barua ya Mabadiliko ya Ramani

NFIP (National Flood Insurance Program) – Mpango wa Bima ya Mafuriko wa Taifa

SFHA (Special Flood Hazard Area) – Eneo Maalum la Hatari ya Mafuriko



Changanua msimbo wa QR ili utembelee ukurasa wa wavuti wa Taarifa za Ramani ya Henrico ili upate maelezo zaidi.



Henrico County
VIRGINIA

5. Lebo tofauti za maeneo zinamaanisha nini?

Jedwali lililo hapa chini linatoa ufafanuzi wa lebo za maeneo ya mafuriko yanayopatikana kwenye ramani za mafuriko katika Kaunti ya Henrico.

KIWANGO CHA HATARI	ENEO LA HATARI YA MAFURIKO
Hatari Kubwa ya Mafuriko	Eneo la AE na A. Mali katika maeneo haya zina uwezekano wa asilimia 1 wa kuathiriwa na mafuriko katika mwaka wowote. Maeneo haya pia yajulikana kama SFHA au maeneo tambarare ya mafuriko ya miaka 100. Masharti ya usimamizi yanatumika kwa maendeleo yote yanayofanyika katika maeneo haya, na ni lazima wamiliki wa nyumba waliochukua mkopo wa nyumba unaodhibitiwa na serikali wanunue bima ya mafuriko. Kuna uwezekano wa asilimia 26 wa kutokea kwa mafuriko katika eneo la mafuriko ya hatari juu kwa kipindi cha mkopo wa nyumba wa miaka 30.
Hatari ya Mafuriko ya Kiwango cha Wastani	Eneo la X Lililoangaziwa. Mali hizi zina uwezo wa asilimia 0.2 wa kutokea kwa mafuriko katika mwaka wowote. Maeneo haya pia yanarejelewa kama eneo tambarare la mafuriko ya miaka 500. Baadhi ya masharti ya udhibiti yanatumika katika eneo hili kwa ajili ya kurefusha majengo na vifaa muhimu.
Hatari ya Mafuriko ya Kiwango cha Chini	Eneo la X (ambalo halijaangaziwa). Mali hizi ziko katika eneo la hatari ya kiwango cha chini kwa ujumla. Hatari katika maeneo haya ni ya kiwango cha chini, lakini bado ipo.

6. Inamaanisha nini kusema kwamba hatari yangu ya mafuriko imeongezeka?

Mali ambazo zimetambuliwa kuwa na ongezeko la hatari ya mafuriko ni pamoja na hali zifuatazo:

- Ardhi zilizo na eneo la SFHA la FEMA linalozidi kuwa kubwa, kumaanisha eneo la SFHA la FEMA linaendelea kuvamia zaidi ardhi hiyo katika angalau eneo moja.
- Ardhi zilizo na eneo la SFHA la Jamii ambazo zina eneo la SFHA la FEMA linalozidi kuwa kubwa, kumaanisha eneo la SFHA la FEMA linaendelea kuvamia zaidi ardhi hiyo katika angalau eneo moja.
- Ardhi zilizo na eneo la SFHA la Jamii ambapo eneo la SFHA la FEMA linawekwa kwenye ramani kwa mara ya kwanza.
- Ardhi zisizo na eneo la SFHA la FEMA au la Jamii ambapo eneo la SFHA la FEMA linawekwa kwenye ramani kwa mara ya kwanza.

Katika baadhi ya hali, kunaweza kuwa na ardhi zilizo na ongezeko na punguo, kwa kuwa mpaka wa eneo tambarare la mafuriko huenda usiwe mstari ulionyooka. Kuongezeka kwa mipaka ya eneo la SFHA inaonyesha kuwa BFE imeongezeka; Hii inamaanisha kuwa maji ya mafuriko yanakadiriwa kufika kiwango cha juu katika mafuriko makubwa kuliko ilivyobainishwa hapo awali. Zaidi ya kuongezeka kwa hatari ya mafuriko, masharti ya ziada ya usimamizi na nununuzi wa bima ya mafuriko yanaweza kutumika kwa mali.

Ingawa huenda isibadilishe viwango vya bima vya Mpango wa Kitaifa wa Bima ya Mafuriko (Nation Flood Insurance Program, NFIP), kutakuwa na masharti mapya ya ujenzi (angalia Swali la 8 la Maswali Yanayoulizwa Sana kwa maelezo zaidi).

7. Itakuwaje ikiwa jengo langu litawekwa katika ramani mpya ya SFHA?

Ikiwa ramani mpya zinaonyesha jengo fulani kwenye mali yako limeongezwa katika eneo la SFHA, utahitajika kisheria kununua bima ya mafuriko ikiwa umechukua mkopo wa nyumba kutoka kwa mkopeshaji anayedhibitiwa au aliye chini ya bima ya serikali, mara tu ramani hizo zitakapoanza kutumika tarehe 25 Aprili 2024. Ikiwa huna mkopo wa nyumba, bado inapendekezwa zaidi ununue bima ya mafuriko, kwa sehemu, kwa sababu **bima nyingi za wamiliki wa nyumba na wapangaji hazilipii uharibifu wa mafuriko**. Ikiwa mali yako iko katika eneo la hatari kubwa, ni muhimu hata zaidi kujilinda kifedha kwa kununua bima ya mafuriko.


Ili kusaidia kupunguza athari za kifedha za mabadiliko ya ramani, NFIP inatoa **punguzo kwa majengo yaliyoongezwa katika ramani mpya** kwa mwaka wa kwanza kwa majengo mapya yaliyoongezwa katika eneo la SFHA. Kisha malipo ya bima yataongezeka polepole kila mwaka hadi yatakapofikia malipo ya bima ya hatari kamili. Ukinunua bima ya mafuriko isiyoyana NFIP kutoka kwa mtoa huduma wa kibinafsi, anaweza kuwa na sheria na masharti tofauti. Zungumza na ajenti wako wa bima kwa maelezo zaidi. Maelezo ya zaidi yanapatikana pia katika www.floodsmart.gov/flood-map-updates.

Zaidi ya hayo, masharti ya kibali cha eneo tambarare la mafuriko yanatumika kwa majengo yaliyo katika eneo la SFHA, na kunaweza kuwa na masharti kuhusu maboresho unayoweza kufanya, kama vile kuongezeka (angalia Swali la 9 la sehemu ya Maswali Yanayoulizwa Sana kwa maelezo zaidi).

8. Mali yangu iko katika eneo la SFHA la Jamii, ni maelezo gani ninayohitaji kujua?

Eneo la SFHA la Kaunti ya Henrico linajumuisha maeneo ya FEMA na SFHA ya Jamii. Maeneo haya ni eneo hatari la mafuriko na yanategemea masharti ya maendeleo yaliyowekwa katika Sheria ya Maeneo Tambarare ya Mafuriko ya Kaunti (Floodplain Ordinance). Kusudi la Sheria ya Maeneo Tambarare ya Mafuriko ni kuendeleza na kulinda afya, usalama, na ustawi wa jumla wa wakazi wa Henrico na kupunguza hasara za mafuriko. Ikiwa una maswali kuhusu unachoweza au usichoweza kufanya kwenye mali yako ndani au karibu na eneo la SFHA, wasiliana na Huduma yetu ya Usaidizi kwa nambari 804-501-7463. Masasisho ya maeneo ya SFHA ya Jamii yanashughulikiwa na yanatarajiwa kukamilika mwaka wa 2025. Pata maelezo zaidi katika henrico.gov/works/design/floodplain/map-updates.

Ingawa bima ya mafuriko si ya lazima katika maeneo ya SFHA ya Jamii ikiwa una mkopo wa nyumba uliochukua kutoka kwa mkopeshaji anayedhibitiwa au aliye chini ya bima ya serikali, inapendekezwa sana kwa sababu bima nyingi za wamiliki wa nyumba na wapangaji hazilipii uharibifu wa mafuriko.



Zaidi ya asilimia 40 ya madai ya mafuriko hutoka nje ya maeneo ambayo ni sharti bima inunuliwe.



Changanua msimbo wa QR ili utembelee ukurasa wa wavuti wa Taarifa za Ramani ya Henrico ili upate maelezo zaidi.



Henrico County
VIRGINIA

9. Ni masharti gani ya kibali yanatumika kwa mali zinazopatikana katika eneo la hatari kubwa?

Maendeleo yote yanayofanywa ndani na karibu na eneo la SFHA lazima yatimize masharti ya Sheria ya Mafuriko ya Kaunti ya Henrico (Henrico County Floodplain Ordinance) (Sheria ya Kaunti ya Henrico Sura ya 10, Kifungu cha 1). Karibu na eneo la SFHA inamaanisha kuwa maendeleo yanafanyika ndani ya futi 40 kutoka katika eneo la SFHA au ndani ya eneo la mafuriko ya miaka 500.

Kabla hujajenga, kujaza au kubadilisha ardhi au jengo lako lililo kwenye ardhi yako, lazima upate Kibali cha Mafuriko ili kuendeleza hali ya kutii Sheria ya Mafuriko ya Kaunti. Kusudi la Sheria ya Eneo Tambarare la Mafuriko (Floodplain Ordinance) ni kuendeleza na kulinda afya, usalama na ustawi wa jumla wa wakazi wa Henrico na kupunguza hasara za mafuriko. Unapaswa kujua:

- Kujaza ardhi hakuruhusiwi ndani ya eneo la SFHA.
- Hakuna nyumba mpya za makazi zinazoruhusiwa kujengwa ndani ya eneo la SFHA au ndani ya futi 15 kutoka katika eneo la SFHA, na nyumba za makazi zilizo katika maeneo haya hazipaswi kupanuliwa.
- Nyumba mpya zisizo za makazi katika eneo la SFHA zinahitajika kuwa na sakafu za msingi zilizoinuka angalau futi mbili juu ya BFE. Uinujaji huu wa ziada, au mwinuko, ni mbinu ya ziada ya ulinzi kutokana na mafuriko na inaweza kusababisha malipo ya chini ya bima ya mafuriko.
- Majengo yote yaliyo karibu na eneo la SFHA, kumaanisha yako ndani ya futi 40 kutoka kwa eneo la SFHA au ndani ya eneo la mafuriko ya miaka 500, lazima yawe sakafu za msingi zilizoinuka kwa futi moja juu ya BFE.
- Vyeti vya Mwinuko vinavyoonyesha miinuko ya sakafu vinahitajika kwa majengo yaliyo ndani na karibu na eneo la SFHA.
- Cheti cha Kutoinuka, kilichotiwa saina na kupigwa muhuri na Mhandisi Mtaalamu aliyesajiliwa katika VA, kinahitajika kwa majengo yote yanayojengwa katika eneo la SFHA kuonyesha kwamba hayawezi kungeza mwinuko wa mafuriko.

Tembelea henrico.gov/works/design/floodplain/map-updates au piga simu au tuma barua pepe kwa Huduma ya Usaidizi ya Kaunti ya Henrico kwa nambari 804-501-7463 au flood@henrico.us ili upate maelezo zaidi.

10. Nyumba au biashara iko katika eneo la hatari kubwa ya mafuriko. Ninapaswa kufanya nini ikiwa ninataka kujenga jengo la ziada au kuliboresha?

Lazima uanze kwa kuomba Kibali cha Ujenzi katika Eneo Tambarare la Mafuriko (Floodplain Development Permit) ili kutii masharti ya ujenzi katika eneo tambarare la mafuriko na kusaidia kuepuka makosa ya gharama kubwa. Nyumba za makazi zilizo katika eneo la SFHA hazipaswi kupanuliwa, lakini maboresho mengine yanaweza kuruhusiwa, kama vile ukarabati wa ndani. Nyumba zisizo za makazi zinaweza kupanuliwa ikiwa masharti yote ya sheria yanayotumika yanaweza kutimizwa.

Kwa majengo yote yanayoboreshwa, thamani ya uboreshaji (urekebishaji, mabadiliko, ukarabati, kujenga upya, nk) haipaswi kuwa sawa au kuzidi asilimia 50 ya thamani ya sokoni ya jengo lililopo. Maboresho yenye thamani ya chini ya asilimia 50 hayapaswi kungeza hali ya kutotii masharti ya jengo.

Nyongeza na/au maboresho mengine yenye thamani ya asilimia 50 au zaidi ya thamani ya sokoni ya jengo lililopo yanazingatiwa kuwa **maboresho makubwa**. Katika hali kama hizo, jengo nzima lazima lishughulikiwe ili kutii masharti ya Sheria ya sasa ya Eneo Tambarare la Mafuriko na Masharti ya Sheria za Ujenzi.

11. Ni nini kitatokea ikiwa jengo langu sasa linaonyeshwa katika eneo la hatari ya kiwango cha wastani au ya kiwango cha chini, badala ya eneo la hatari kubwa?

Ikiwa jengo lako litatambuliwa upya kuwa katika eneo la hatari ya kiwango cha wastani au ya kiwango cha chini wakati ramani zinaanza kutumika, hutahitajika kisheria kununua bima ya mafuriko ikiwa una mkopo wa nyumba uliochukua kutoka kwa mkopeshaji anayedhibitiwa au anayelindwa na bima ya serikali. Hata hivyo, mkopeshaji wako bado anaweza kukuhitaji uwe na bima ya mafuriko.

Ingawa hatari yako ya mafuriko inaweza kuwa ya kiwango cha wastani hadi kiwango cha chini, bado jengo lako liko hatarini. Bima ya mafuriko bado inapendekezwa zaidi katika maeneo haya. Isitoshe, wamiliki wa bima ya NFIP walio nje ya maeneo ya hatari kubwa ya mafuriko yaliyobainishwa huwasilisha zaidi ya asilimia 40 ya madai yote ya bima ya mafuriko ya NFIP.

Majengo katika maeneo haya bado yanaweza kutegemea masharti ya udhibiti ikiwa yanapatikana katika eneo tambarare la mafuriko ya miaka 500 au ndani ya futi 40 kutoka katika eneo la SFHA.

Maelezo

Mwinuko wa Mafuriko ya Msingi ni urefu (juu ya kiwango cha bahari) ambao maji ya mafuriko yanakadiriwa kufikia au kupita katika tukio la mafuriko na angalau uwezekano wa asilimia 1 wa kutokea katika mwaka wowote, pia inajulikana kama eneo la SFHA au eneo tambarare la mafuriko ya miaka 100.

Maendeleo - Mabadiliko yoyote yanayofanywa na mwanadamu kwa ardhi au nyumba yoyote.

Mwinuko - Urefu wa ziada wa usalama, unaonyeshwa kwa futi juu ya mwinuko mahususi wa mafuriko, kwa kawaida ni BFE. Kaunti ya Henrico imeweka masharti ya mwinuko wa futi 2 ndani ya eneo la SFHA na masharti ya mwinuko wa futi 1 katika maeneo yaliyo karibu na eneo la SFHA.



Changua msimbo wa QR ili utembelee ukurasa wa wavuti wa Taarifa za Ramani ya Henrico ili upate maelezo zaidi.



Henrico County
VIRGINIA

12. Itakuwaje ikiwa nyumba au biashara yangu imewekwa katika eneo la hatari kubwa, lakini ninaamini kuwa imewekwa kimakosa?

Ikiwa unafikiria mali yako imewekwa kimakosa katika eneo la hatari kubwa, unaweza kutuma ombi kwa FEMA ili LOMC ifanywe. LOMC inaonyesha mabadiliko/marekebisha rasmi kwa FIRM inayotumika. Ikiwa ombi la LOMC litakubalika, unaweza kustahili kulipa malipo ya chini ya bima ya mafuriko au chaguo la kutonunua bima ya mafuriko. Data ya kiufundi lazima itolewe ili kuunga mkono madai yoyote kwamba nyumba/ardhi imewekwa katika eneo lisilo sahihi, kama vile data ya mwinuko wa ardhi na/au tafiti za mafuriko zilizorekebishwa. Ili upate maelezo zaidi kuhusu LOMC za FEMA, tembelea www.fema.gov/letter-map-changes.

13. Ninakodisha nyumba/ardhi katika eneo lenye hatari kubwa. Je, ninapaswa kuwa na Bima ya Mafuriko?

Ikiwa unakodisha nyumba au biashara kwenye ardhi inayopatikana katika eneo la SFHA, kumbuka kuwa ingawa mwenye nyumba yako anaweza kuwa na bima ya mafuriko ya kulinda jengo lake, bima hiyo haitalinda mali yako binafsi. Ni bima tofauti pekee ya mafuriko inayoweza kulinda vitu vilivyoharibiwa katika mafuriko. Jilinde kwa kununua bima ya mafuriko ya kulinda mali binafsi. Ajenti wako wa bima anaweza kukusaidia kupata bima na kujibu maswali yako.

14. Ninawezaje kulinda mali yangu kutokana na mafuriko?

Malipo ya bima ya mafuriko yanategemea sababu kadhaa, lakini kuna hatua kadhaa ambazo unaweza kuchukua ili kufanya bima ya mafuriko iwe nafuu zaidi kila mwaka:

- **Punguza hatari yako ya mafuriko.** Malipo unayolipa kwa bima ya mafuriko ya NFIP mara nyingi huhusiana sana na hatari ya mafuriko inayohusishwa na mali yako. Kupunguza hatari yako ya mafuriko hailindi tu mali yako kutokana na uharibifu wa mafuriko lakini pia inaweza kusaidia kupunguza gharama za bima.
- **Toa cheti cha mwinuko.** Ingawa hakihitajiki wakati wa kununua bima, kinaweza kusaidia ajenti wako wa bima kukupa bima ya bei nafuu.
- **Chagua kiwango cha juu cha gharama ya kulipa mwenyewe.** Ukichagua kiwango cha juu cha gharama ya kulipa mwenyewe utapunguza malipo yako ya bima, lakini inamaanisha utahitaji kulipia mwenyewe gharama zaidi za kujenga upya. Ukiongeza kiwango cha gharama ya kulipa mwenyewe kwenye bima yako hadi kiasi cha juu zaidi cha \$10,000 unaweza kupunguza malipo yako ya bima ya kila mwaka hadi asilimia 40. Kumbuka, kutumia kiwango cha juu cha gharama ya kulipa mwenyewe huenda isifae au kuruhusiwa kwa kila mtu.

Tembelea <https://www.floodsmart.gov/how-can-i-pay-less> ili upate maelezo zaidi. Kaunti ya Henrico kwa sasa inajitahidi kujunga na Mpango wa CRS, ambao utatoa punguzo la malipo ya bima ya mafuriko kwa wamiliki wote wa bima za NFIP katika Kaunti. Hii inatarajiwa kuanza kutumika mnamo Oktoba 2024.

15. Ni sheria gani za kutoa maelezo zinazotumika wakati wa kununua mali katika eneo la mafuriko?

Virginia ni jimbo la "Mnunuzi Tahadhari (Buyer Beware)". Hii inamaanisha kuwa wauzaji hawatakiwi kutoa maelezo yoyote yanayohusiana na hatari ya mafuriko ya mali, ukaribu na eneo la mafuriko linalodhibitiwa, bima ya mafuriko au uharibifu wa awali uliosababishwa na mafuriko. Wanunuzi wote watarajiwa lazima wafanye uchunguzi wao wa msingi kuhusu mali kabla ya kununua, ikiwa ni pamoja na kuangalia kiwango cha hatari ya kuathiriwa na mafuriko cha mali na sheria zozote za Nchi au Kaunti zinazotumika kwa mali kulingana na mahali inapopatikana katika eneo la SFHA.


Sheria ya kubadilisha masharti ya kutoa maelezo kuhusu uwezekano wa mali kuathiriwa na mafuriko iliwasilishwa hapo awali kwa Bunge la Nchi, hivi majuzi katika Kikao cha 2024, lakini sheria hii haijapitishwa. Ikiwa una wasiwasi kuhusu masharti ya kutoa maelezo kuhusu uwezekano wa mali kuathiriwa na mafuriko katika jimbo la Virginia, unaweza kuwasiliana na wawakilishi wa Bunge na Seneti kuhusu suala hili. Unaweza kumtambua mbunge wako hapa: whosmy.virginiageneralassembly.gov.


16. Ni nyenzo gani za ziada zinazopatikana?


Iluatayo ni orodha ya nyenzo na maelezo ya mawasiliano unazoweza kuwasiliana nazo ukiwa na maswali zaidi.

- Tembelea henrico.gov/works/design/floodplain/map-updates ili uone ramani zilizosashishwa na zinazotumika kwa sasa na upate maelezo kuhusu mradi na matukio yajayo
- FloodSmart.gov: Maelezo ya jumla kuhusu bima ya mafuriko ya NFIP
- Mabadiliko ya Ramani na Bima ya Mafuriko: Mambo Ambayo Wamiliki wa mali Wanapaswa Kujua: Kijitabu cha Maelezo cha FEMA (<https://bit.ly/Property-Owners>)
- Ukiwa na maswali ya jumla kuhusu bima ya mafuriko na ramani ya hatari ya mafuriko, piga simu kwa FEMA Mapping and Insurance eXchange (FMIX) kwa nambari 1-877-FEMA MAP (1-877-336-2627) au tuma barua pepe kupitia FEMA-FMIX@fema.dhs.gov. FMIX hufunguliwa kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, saa mbili asubuhi (8 a.m.) hadi saa moja jioni (7:00 p.m.) majira ya ET.

**UNAHITAJI MSAADA?
WASILIANA NA HUDUMA YA USAIDIZI YA
TAARIFA ZA RAMANI YA MAFURIKO YA HENRICO**

 Nambari ya simu: 804-501-7463

 Barua pepe: flood@henrico.gov

 Huduma za Tafsiri Zinapatikana



Changanua msimbo wa QR ili utembelee ukurasa wa wavuti wa Taarifa za Ramani ya Henrico ili upate maelezo zaidi.



Henrico County
VIRGINIA